**JAMHURI YA MUUNGO WA TANZANIA**

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

**MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A**

**610** **UALIMU**

**Muda: Saa 3.** **Year: 2024**

---

**Maelekezo**

1. Karatasi hii ina Sehemu **A** na **B** zenye jumla ya maswali **kumi na manne (14).**
2. Jibu maswali **yote** kutoka Sehemu **A** na maswali **manne (4)** kutoka Sehemu **B**.
3. Sehemu **A** ina alama **arobaini (40)** na Sehemu **B** ina alama sitini **(60).**
4. Simu za mkononi **haziruhusiwi** ndani ya chumba cha mtihani.
5. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

maktaba.tetea.org
TETEA


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

## SEHEMU A (Alama 40)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

1. bainisha mambo manne ya kuzingatia inapotumika mbinu ya mshauri kuwa kiini cha ushauri wakati wa unasihi.
2. eleza kwa ufupi hoja nne zinazoonesha ufanano kati ya ushauri nasaha wa jadi na ushauri nasaha wa kisasa.
3. fafanua ngazi nne za Nyanja ya Stadi kwa kufuata mtiririko kutoka ngazi ya chini hadi ngazi ya juu.
4. bainisha mambo manne muhimu katika kipengele cha taaluma ambayo yanatakiwa kuingizwa kwenye kumbukumbu za maendeleo ya wanafunzi.
5. eleza kwa ufupi faida mbili na hasara mbili za kutumia mbinu ya kusoma kwa sauti katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji.
6. toa matukio manne yaliyofanyika kama sehemu ya kuimarisha elimu ya watu wazima nchini Tanzania.
7. tumia hoja nne kueleza kwa ufupi jinsi elimu inavyoweza kutumika kama chombo cha ukandamizaji kama ilivyoelezwa na Paulo Freire.
8. eleza kwa ufupi misingi minne ya kufuata katika upangaji wa maswali ya mtihani.
9. toa hoja nne za kuzingatia katika kuhariri vitabu vya kiongozi cha mwalimu.
10. eleza kwa ufupi majukumu manne ya Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi.

## SEHEMU B (Alama 40)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

11. tumia hoja sita kuonesha mchango wa sifa zilizorithiwa kwenye haiba ya mtoto.
12. chambua vipengele sita vya mtaala ambavyo huwawezesha walimu kujua majukumu yao katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji.
13. fafanua manufaa matatu na mapungufu matatu ya maswali ya kuchagua jibu sahihi.
14. toae hoja sita zinazoeleza umuhimu wa walimu wa elimu ya msingi kujiendeleza kitaaluma.


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org